




Kongamano la  
Kiswahili



UNIVERSITÄT  
BAYREUTH

Literaturen in afrikanischen Sprachen | 95440 Bayreuth | Tel.: +49 921 55-3550 Fax: +49 921 55-3641  
Email: swahili@uni-bayreuth.de | [http://www.afrikanistik.uni-bayreuth.de/de/colloq/swahili\\_colloq/index.html](http://www.afrikanistik.uni-bayreuth.de/de/colloq/swahili_colloq/index.html)

## Kongamano la Thelathini na moja la Kiswahili Bayreuth

Iwalewahaus, tarehe 11 hadi 13 Mei 2018

Tarehe 13 Machi 2018

Waalikwa Wapendwa – Mabibi na Mabwana,

Kwa mara nyingine tunawashukuruni sana kwa kuuitika mwito wetu. Kwa furaha tumepokea mihutasari na makala nyingi kutoka kwenu. Kukutana nanyi nyote hapa kwetu itakuwa furaha hata zaidi. Karibuni sana!

Katika barua hii ya pili tunawatumia pia ratiba ya kongamano la mwaka huu, kama ilivyo kwa wakati huu. Kongamano la mwaka huu litafanyika **Iwalewahaus**. Anwani ni: Iwalewahaus, Wölfelstr. 2, 95444 Bayreuth. Kongamano litaanza **Ijumaa tarehe 11**, saa mbili na nusu asubuhi. Kujisajili kutagharimu Euro 15 kwa wasio wanafunzi/Euro 10 kwa wanafunzi wageni.

Siku moja kabla ya Kongamano, yaani **Alhamisi tarehe 10**, saa moja, tutakutana kwa chakula cha jioni kama ilivyo kawaida yetu. Mkahawa unaitwa ‘Hua Hin’ (anwani yake ni: Ludwigstr. 30; <http://www.thai-huahin.de/>). Tafadhali eleweni kwamba hatutaweza kuwalipia siku hiyo.

Bali na hayo kongamano letu la mwaka huu lina mambo ya zaidi: **Ijumaa** asubuhi, kabla ya mawasilisho, Prof. Kithaka wa Mberia atasoma baadhi ya mashairi yake. Jioni, kwa furaha kubwa tutawakaribisha washindi wa kwanza wa tuzo la Mabati-Cornell (*Mabati Cornell Kiswahili Prize for African Literature* <http://kiswahiliprize.cornell.edu/>). Kwa upande wa riwaya, Ali Hilal Ali atasoma riwaya yake *Mmeza Fupa* na kwa upande wa ushairi, Dotto Rangimoto atasoma baadhi ya mashairi ya diwani yake *Mwanangu Rudi Nyumbani*. Siku ya **Jumamosi**, kutakuwa na kikao pamoja na wanafunzi wa BIGSAS chenye madhumuni ya kuchungua umuhimu wa utafiti katika ujao wa taaluma za lugha na fasihi za Kiafrika/Afrika. Jioni, Dr. Ndirangu Wachanga atatuonyesha filamu aliyoitayarisha kumhusu Ngugi wa Thiong’o. Siku ya **Jumapili**, Lydia Kasese, mshairi kutoka Dar es Salaam, atasoma baadhi ya mashairi yake.

Iwapa kuna maswali yoyote, msisite kuwasiliana nasi katika hapa: [swahili@uni-bayreuth.de](mailto:swahili@uni-bayreuth.de)

Karibuni sana!

Ni sisi wenyeji wenu,

Clarissa Vierke, Nikitta Adjirakor, Duncan Tarrant na Fred Bosire